

**MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KANGEMA– 2016****KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASIHI****1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'****USHAIRI**

Ole wangu! Ole wangu, nisikize Mola wangu,  
Lipokee ombi langu, wanisikize wenzangu,  
Washike ujumbe wangu, uloleta Mola kwangu,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Amri kumi za Mola, mumekwisha zikiuka  
Ndipo hamuwezi lala, mumekwisha vurugika,  
Mumemsahau Mola, ndipo nanyi mwasumbuka,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Mwaabudu mashetani, ushirikina ni mwingi,  
Munaiba hadharani, waongo nao ni wengi,  
Mwajawa na taraghani, na wazimu mwingi,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora,

Mwauana ovyoovyo, mwasemana ndivyo siyyo,  
Fitina nazo zilivyo, mwarogana vivyo hivyo,  
Matusi ni vile siyyo, munaisha ka isivyo,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Kuna dawa za kulevya, na hata pembe haramu,  
Na ukimwi nakujavya, unaua wanadamu,  
Na mimba nazo kuavya, watoto ni marehemu,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Wengine nao hudai, waoe jinisi moja,  
Ati mwingine hafai, heri sawia ya mja,  
Haya maoni ni hoi, tupinge kila mmoja,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.  
Ploti mwazinyakua, na viwanja vya mipira,  
Makaburi mwala pia, mabibi mwateka nyara,  
Ibada zikifikia, mwafurika kwa majira  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Wengi tuwachagua, si viongozi ni waizi,  
Tamaa walio nao, yaongoza maamuzi,  
Mishahara ile yao, huongezwa kila mwezi,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Usalama hatunao, wasiwasi umezidi,  
Waja kiwa makazio, huogopa magaidi,  
Mabomu walipua, huruma wamekaidi,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

Beti kumi namaliza, dua yangu imetimu,  
Mungu amekwisha anza, kuhukumu mwanadamu,  
Wote walojipotoza, waiepuke hukumu,  
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

**MASWALI**

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)  
 (b) Shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari kadhaa. Taja na ueleze bahari zozote tatu. (alama 3)  
 (c) Taja na ueleze mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika ubeti **wa kwanza**. (alama 3)  
 (d) Eleza sababu ya mshairi kutumia alama ya ritifaa katika ubeti wa nne (alama 2)  
 (e) Tambua uhuru wa kishairi uliotumika katika ubeti wa tisa mshororo wa tatu na ueleze umuhimu wake. (alama 2)

- (f) Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. (alama 4)  
 (g) Taja mifano mitatu ya uozo anaolalamikia mwandishi. (alama 3)  
 (h) Eleza toni ya mwandishi. (alama 2)

**SEHEMU YA B****TAMTHILIA:****Mstahiki Meya : Timothy M. Arege****Jibu swali la 2 au la 3**

2. Mbona isiwe kweli? Wewe panga uwaleta tule matunda ya jasho letu nao watoto.  
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
 (b) Eleza mbinu mbili za uandishi katika dondoo hili. (alama 2)  
 (c) Eleza yaliyopangwa baada ya usemi huu. (alama 14)
3. Fafanua jinsi maudhui ya unafiki yamejidhihirisha katika tamthilia ya Mstahiki Meya, ukirejelea wahusika wowote watano. (alama 20)

**SEHEMU YA C****RIWAYA:****Kidagaa kimemwozea : Ken Walibora****Jibu swali la 4 au la 5**

4. Mtoto ni mtoto hata likiwa bonge la nyama. Mtu hupata ajaliwalo sio alitakalo.  
 (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
 (b) Eleza tamathali ya lugha iliyotumika katika usemi huu. (alama 2)  
 (c) Ukirejelea riwaya thibitisha kuwa mtu hupata ajaliwalo silo alitakalo. (alama 14)
5. "Ndoto za uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi, jinamizi inayowafanya wazalendo kulia Kidagaa kimetuozea". Ukirejelea riwaya eleza sababu za wazalendo kulia Kidagaa kimetuozea. (alama 20)

**SEHEMU YA D:****HADITHI FUPI****Damn Nyeusi na Hadithi nyingine : Ken Walibora na Said A. Mohamed****Jibu swali la 6 au la 7**

6. "Ingawa walifahamu sababu ya kuitwa pale mpango uliokuwepo ulikuwa usiku wa giza."  
 (a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)  
 (b) Eleza tamathali iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)  
 (c) Onyesha vile wahusika mbalimbali hadithini waiivyoathiriwa na sababu ya kuitwa pale. (alama 14)
7. Uozo katika jamii ni maudhui yaliyoshughulikiwa pakubwa katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. Kwa kurejelea hadithi zozote tano fafanua kauli hii. (alama 20)

**SEHEMU YA E:****FASIHI SIMULIZI**

8. a) i) Eleza maana ya vitendawili. (alama 2)  
 ii) Chambua muundo wa vitendawili ukizingatia hatua muhimu katika utendaji. (alama 7)  
 b) i) Ulumbi ni nini? (alama 2)  
 ii) Eleza sifa zozote tano za ulumbi. (alama 5)  
 iii) Ulumbi hutekeleza majukumu gani katika jamii. (alama 4)